**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA**
*(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)*

Unapojibu tafadhali taja:

**Kumb.Na MDC/L.40/9/157** Tarehe 29/01/2024

MKURUGENZI,
KAMPUNI YA CANUCK
S. L. P. 846,
**MWANZA.**

**KUH: OMBI LA KUWASILISHA CHETI (CERTIFICATE OF INCENTIVES) CHA ENEO LA LESENI YA UCHIMBAJI MADINI -CANUCK LILIPO MWAKATA.**

Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu.

1. Itakumbukwa kampuni ya Canuck inafanya shughuli zake za uchimbaji madini katika eneo la Mwakata, kijiji cha Mwanguhun'gwa katika Halmashauri ya wilaya Msalala.

2. Kampuni hii ilipata eneo hili kwa kuwalipa fidia wananchi waliokuwa wanamiliki maeneo hayo kiasili. Baada ya kupata eneo hilo, kampuni tajwa imeweza kuliandalia mchoro wa mipango miji pamoja na kulifanyia upimaji wa viwanja. Na sasa kampuni yako iko katika hatua ya umilikishaji kisheria, ambapo itamilikishwa viwanja saba kama ifuatavyo:

| S/NO | NAMBA YA KIWANJA | KITALU | ENEO |
|---|---|---|---|
| 1 | 19 | F | MWAKATA - MSALALA |
| 2 | 20 na 21 | F | MWAKATA - MSALALA |
| 3 | 22 | F | MWAKATA - MSALALA |
| 4 | 23, 24 na 25 | F | MWAKATA - MSALALA |

3. Zoezi la umilikishaji kwa kampuni ya Canuck linapitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (Tanzania Investment Centre) kwa ushirikiano na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Hivyo **tunaomba uwasilishe Cheti (Certificate of Incentives)** idara ya ardhi Msalala chenye taarifa za viwanja utakavyomilikishwa kisheria kama jedwali tajwa hapo juu linavyoeleza ili taratibu za umilikishaji ziweze kuendelea. Naambatanisha nakala ya ramani ndogo (deed plan) kwa rejea.

4. Nawasilisha.

L. F. Ndenga

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
MSALALA

**K.n.y MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**MSALALA**

MkoawaShinyanga, Kata yaNtobo, S.L.P 16 **KAHAMA**. Simu: 028–2710182, Nukushi: 028–2710504,
Barua pepe: ded@msalaladc.go.tz, Tovuti: www.msalaladc.go.tz

CamScanner